

HALMASHAURI YA MJI NEWALA

BARUA ZOTE ZLANDIKWE KWA MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI NEWALA

Simu Na: (+255) 023 2410673



Mkurugenzi wa Mji,
S.L.P 39,
NEWALA

Unapojibutafadhalitaja

Kumb.Na.NTC/I.20/05/133

24/06/2020

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Newala anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa kazi ifuatayo:-

MTENDAJI WA KIJIKI III – NAFASI (1)

SIFA ZA MWOMBAJI:-

- Mwombaji awe amefaulu kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyefuzu mafunzo ya Astashada Cheti "NTA Level 5" katika fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI:-

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao
- Kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia/Sera, Sheria na Taratibu katika Kijiji
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji

- Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi
- Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji.

MSHAHARA:-


- Cheo cha Mtendaji wa Kijiji daraja la III kina Mshahara wa TGS B kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA:-

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Mwombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma apitishe barua yake ya maombi kwa Mwajiri wake.
- Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya elimu na taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- "Testimonials" Provisional results", Statement of results" nk hazitakubalika.
- Waombaji waweke picha moja ya "passport size" katika barua zao za maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NECTA.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 07/07/2020 saa 9.30 alasiri
- Barua zote zitumwe kwa anuani iliyopo hapa chini.

**MKURUGENZI WA MJI,
HALMASHAURI YA MJI,
S.L.P. 39,
NEWALA.**

NB:- Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri ya Mji
Newala ambayo ni info@newalatc.go.tz



Andrew Frank Mgaya,,
**MKURUGENZI WA MJI,
NEWALA.**

- Nakala:-
- Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa umma,
Jengo la Utumishi,
8 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 63100,
11404 DAR ES SALAAM.
 - " Tovuti ya Halmashauri,
www.newalatc.go.tz
 - " Mbao za Mtangazo